# Matumizi ya Takriri ya Kimsamiati katika Ushairi wa Kiswahili[1]

**E. Lyimo**

**Ikisiri**

Takriri ni kipengele ambacho kimeelezwa kuwa ni muhimu katika kazi za fasihi hasa katika utanzu wa ushairi (Finnegan 1977, Leech 1969, Kahigi na Mulokozi 1979). Vile vile, kipengele hiki cha takriri kimeelezwa na wataalamu mbalimbali kuwa kinapatikana katika viwango vyote vya kiisimu ambavyo ni kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia kisemantiki, na kipragimatiki. Pamoja na ukweli huu, ushahidi unaotokana na tahakiki mbalimbali za kazi za fasihi unaonesha kuwa baadhi ya wahakiki wa kazi hizi ama hawakukizingatia kabisa kipengele hiki cha takriri katika uhakiki wao, au kipengele hiki kimeshughulikiwa lakini si kwa kina. Kwa mfano kuna wahakiki ambao hawakukitaja kabisa kipengele hiki katika tahakiki zao; wengine wamekitaja tu bila kukichambua; na wachache wamejaribu kukichambua ila si kwa kina (taz. Lyimo, 2004 kwa ufafanuzi zaidi). Makala hii inachambua matumizi ya takriri katika utanzu wa ushairi. Lengo ni kuonesha umuhimu wa takriri katika utanzu huu kama kipengele cha kiushikamani na kipengele cha kimtindo katika ushairi wa Kiswahili. Makala hii inazingatia takriri katika kiwango cha kileksia/kimsamiati kwa kutumia mkabala wa elimu-mitindo na inatumia mashairi mawili na utenzi mmoja wa Kiswahili kama mifano.

## Utangulizi

Makala hii inachambua takriri ya kimsamiati katika ushairi wa Kiswahili kwa kutumia mkabala wa elimu-mitindo. Elimu-mitindo ni mkabala au taaluma inayotumia mbinu za kiisimu katika uhakiki (Leech and Short 1981:13). Mkabala huu, licha ya kuangalia kile kinachowasilishwa, unaangalia pia jinsi kinavyowasilishwa. Kwa hivi, mkabala wa elimu-mitindo unachunguza zaidi lugha na vipengele vyake katika kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi.

Takriri si dhana ngeni; ni dhana ambayo imezoeleka katika uwanja wa fasihi na katika nyanja nyinginezo. Kutokana na kuzoeleka huku, baadhi ya waandishi wanaiona kama istilahi ya kawaida tu na wala si istilahi ambayo inahitaji kufafanuliwa (Persson 1974).

---

[1] Kazi hii msingi wake ni Tasnifu yangu ya Uzamili Reiteration in Kiswahili Poetry (2004), chini ya Msimamizi wangu Prof. Kulikoyela Kahigi.

TUKI (2004) inafafanua takriri kama umbo linalorudiwa katika kuliandika, na kama kibwagizo au mkarara. Katika kufafanua zaidi fasili hii, Mulokozi na Kahigi (1979:40) wanaeleza kuwa takriri ni marudiorudio ya sauti, silabi, neno, sentensi, wazo au ridhimu fulani ili kuleta athari maalumu na maana maalumu.

Kwa kuchunguza fasili hizi, tunaona kuwa zimebeba kiini cha dhana 'takriri', ambacho ni 'marudiorudio'. Marudiorudio hayo yanaweza kuwa katika darajia mbalimbali kama vile sauti, neno (msamiati), kirai, kishazi sentensi na maana. Kwa hiyo basi, takriri yaweza kujitokeza kwenye viwango vyote vya lugha ambavyo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Makala hii itashughulikia takriri katika kiwango cha kimsamiati. Makala itatoa mwanga kuhusu hali ya uchambuzi wa takriri katika tahakiki za fasihi ya Kiswahili, kisha itafanya uchambuzi wa takriri ya kimsamiati kwa kutumia mifano ya ushairi wa Kiswahili. Makala itatumia mkabala wa Halliday na Hasan (1976) na Kahigi (1997) kuhusu ushikamani.

**Uchambuzi wa Takriri katika Tahakiki za Fasihi ya Kiswahili**

Takriri ni kipengele cha lugha ambacho baadhi ya waandishi wanakitambua kama kipengele muhimu katika ushairi (Taz. Finnegan 1977, Leech 1969, Kahigi na Mulokozi 1976). Licha ya umuhimu huu unaotambuliwa na wataalamu, takriri ni miongoni mwa vipengele vya lugha ambavyo havijachambuliwa kwa kina. Utafiti uliofanywa kwa kupitia tahakiki mbalimbali unaonesha kuwa wapo wahakiki ambao wamechambua maudhui katika kazi za fasihi bila kuzingatia fani hususani lugha. Baadhi yao ni Senkoro (1988), Tandika (1986) na Mlacha (1984). Kwa mfano Tandika alichambua Kuli, Fimbo ya Mnyonge na Shida lakini hakuzungumza cho chote kuhusu fani katika kazi hizi.

Baadhi ya wahakiki wamechambua maudhui na fani ya kazi za kifasihi za Kiswahili lakini kwa upande wa lugha na vipengele vyake yametolewa maelezo mafupi sana ambayo hayakidhi ile umuhimu wa takriri katika kazi hizi. Baadhi ya kazi ambazo zinaonesha hali hii ni kama vile Chacha (1992), Materu, Mushi na Njau (1986), Lihamba, Materu, Mushi na Njau (1986) na Senkoro (1984). Kwa mfano Materu, Mushi na Njau (1986) wamechambua Tendehogo. Katika kipengele cha lugha wahakiki hawa wametoa tu kauli ya jumla kuhusiana na lugha ambayo imetumika katika kitabu hicho kuwa ni Kiswahili Sanifu na Kiswahili chenye athari za Kiarabu na hawakuchambua kipengele chochote kuhusiana na madai yao.

Si hivyo tu, bali wapo wahakiki ambao wamechambua fani na maudhui vikiwemo vipengele vya lugha katika kazi za Kiswahili, lakini hawakuweza japo hata kukitaja kipengele cha takriri miongoni mwa vipengele vilivyoshughulikiwa. Mifano ni Mvungi (1988), Mponda (1988), Senkoro (1988).

**Isitoshe,** baadhi ya wanataaluma wametaja tu takriri bila ufafanuzi au kutoa mifano. Mfano wa wahakiki hawa ni Khatibu (1986) na Sanka (1988).

Aidha, baadhi ya wanataaluma wametaja tu aina za takriri bila kuzifanyia uchambuzi wowote. Mfano Msokile (1986) amechambua Teuzi za Nafsi na katika uchambuzi wake ametaja tu aina mbalimbali za takriri ambazo ni pamoja na takriri mstari, takriri vina, takriri konsonanti, takriri vokali na kituo bahari. Anasema kwamba Teuzi za Nafsi kimejaa aina hizi za takriri. Hata hivyo hakuzichambua.

Picha ya kijumla inayopatikana kuhusu uchambuzi wa takriri inaonesha kuwa wapo wahakiki wa Kiswahili wachache sana kama Mulokozi na Kahigi (1979), King'ei (1987), Mulokozi (1996) na Kahigi (1997), ambao wamejaribu kushughulikia takriri angalau kwa kiasi fulani, ama kama kipengele cha kifasihi au cha kimtindo katika matini za Kiswahili. Kwa mfano Mulokozi na Kahigi (1979) wameangalia aina mbalimbali za takriri na kutoa mifano. Hata hivyo, hawakuonesha jinsi ya kuchambua takriri katika matini au katika kazi fulani ya fasihi kama vile ushairi.

**Mchakato wa Uchambuzi wa Takriri ya Kimsamiati katika Ushairi**

Katika uchambuzi wa takriri katika matini yoyote, mchambuzi anatakiwa kwanza asome matini husika ili aweze kupata maana yake. Pili, lazima mchambuzi awe na ujuzi wa kugundua takriri ambazo anazichambua na kuzitofautisha na aina nyingine za takriri zilizopo katika matini hiyo kwa maana ya hana budi kujiwekea mipaka ili kuepuka kuchambua aina nyinginezo za takriri na kwa lengo la kurahisisha ufafanuzi. Tatu, ni vema kuipa namba mistari yote (kama ni ushairi) au sentensi zote katika matini ili kurahisisha urejelezi wa kile kinachozungumziwa wakati wa uchambuzi wa takriri. Tano, atumie msimbo tofauti kwa kila aina ya takriri anayoichambua. Sita, baada ya kuchambua na kuzibainisha aina zote za takriri za msamiati, lazima afanye zoezi la kuhusisha utokeaji wa aina ya takriri na dhima yake katika matini husika.

**Je, kila Takriri Inafaa Kuchambuliwa?**

Mulokozi na Kahigi (1979:40) wanasema kuwa:

> Takriri inayonufaisha ni ile tu yenye uasili, inayofungamana na muundo na mwendo asilia wa lugha inayohusika, na inayojitokeza kisanaa bila kulazimishwa wala kupachikwa, inayotokana na inayooana na maudhui ya shairi kueleza na kuongeza hisia za mshairi katika kazi yake.

Mawazo ya wataalamu hawa juu kueleza na kuongeza hisia yanaendana na dhana nzima ya mchomozo. Hii ni dhana ya kisaikolojia inayoeleza utokeaji wa wingi wa kipengele fulani katika matini au utokeaji wa kiasi kidogo au kutokujitokeza kabisa kwa kipengele ambacho kilitegemewa kiasi cha kumfanya msomaji au hadhira ijiulize maswali ya "kwa nini?" Kujiuliza swali la "kwa nini?" kunamfanya msomaji atafute maana iliyofichika katika mchomozo huo (Halliday 1971). Kwa maana hii, takriri inayochambuliwa ni ile ambayo imeonekana kuwa ni mchomozo.

Ni vema pia kuelewa kuwa msanii huwa na malengo mbalimbali katika kazi yake na hivyo hutumia mbinu anuwai katika kutimiza malengo yake. Kwa kutambua hili, pindi kipengele kijitokezapo kwa wingi au kwa uchache, mchambuzi lazima makini yake yavutike, na hivyo ujitokezaji huo kuhitaji uchambuzi.

**Uchambuzi wa takriri ya kimsamiati**

Takriri ya kimsamiati huchambuliwa kwa mtazamo wa kiushikamani. Tofauti na aina nyingine za takriri, takriri ya kimsamiati huzingatia marudio ya neno lilelile, matumizi ya sinonimua, neno jumuishi, neno jumuishwa (hiponimia) na neno jumla.

Kabla ya uchambuzi wenyewe ni vema tukafafanua dhana hizi na msimbo uliotumika katika mchakato wa uchambuzi. Tutatoa pia muhtasari wa matini zilizotumika kama data.

**Ufafanuzi wa Dhana**

**Msamiati:** Katika kazi hii ni neno lolote ambalo linaweza kufanya kazi ama ya kisarufi kama vile viunganishi, vihusishi n.k au ya kileksia kama vile kitenzi, nomino n.k.

**Sinonimu**

Hili ni neno ambalo ni kisawe cha neno husika. Sinonimu huweza kutumika badala ya neno husika.

Mfano: **Habari hii inahusu *msichana* mmoja *binti* huyu..........**

Katika mfano huu neno **binti** ni sinonimu, ni kisawe cha neno **msichana**.

**Hiponimu**

Hili ni neno jumuishwa. Neno hili linakuwa na baadhi ya sifa za neno jumuishi ambazo ni pambanuzi.

Mfano: Uhusiano uliopo kati ya maneno **pera, embe, ndimu, papai** na neno **tunda** ni wa ujumuishwa na wa ujumuishi; kwamba pera kama mfano mmojawapo linajumuishwa katika **tunda**. Hivyo, pera ni hiponimi.

**Neno jumuishi**

Hili ni neno ambalo linabeba au linajumuisha sifa au dhana nyinginezo za maneno mengine. Neno **tunda** dhidi ya maneno **pera, embe, ndimu** na **papai** (Angalia mfano wa hapo juu) ni neno jumuishi.

**Neno jumla**

Hili ni neno la kawaida katika lugha ambalo limezoeleka na wazungumzaji ambalo si la pekee na halioneshi uhusiano kam ulioelezwa hapo juu.

Mfano:

> Habari ile ilimhusu kijana mmoja[1]. Kijana huyo alikuwa msichana[2]. Binti huyo alikuwa mzuri kuliko vijana wengine[3]. Hata hivyo uzuri wake ni sawa tu na uzuri wa binadamu wengine[4]

Katika mfano huu kuna marudio ya neno lilelile (kijana) katika sentensi ya 2, matumizi ya sinonimu (binti) badala ya msichana sentensi ya 3, matumizi ya hiponimi (msichana), neno jumuishi (kijana) na neno jumla (binadamu).

Kutokana na ufafanuzi na mifano hii tunaona kuwa, kuna ufungamano kati ya maneno hayo ambao unaleta mtiririko wa mawazo na hivyo kuleta maana. Ushikamani ni sifa kuu ya matini. Ushikamani ni dhana inayoeleza ufungamano wa vipengele kama vile sentensi na aya katika matini.

Mbali ya ushikamani wa kimsamiati pia upo ushikamani wa kisarufi ambao hujumuisha urejezi, ubadala, udondoshaji na uunganishaji. Ushikamani ni muhimu kwa sababu ufafanuzi wa kipengele fulani katika matini hutegemea kuwepo kwa kipengele kingine.

Katika kuchambua takriri ya kimsamiati makala hii itatumia mifano kutoka katika mashairi na utenzi. Mashairi mawili –"Hadithi ya Mzee", na "Nimekaribishwa pombe" na "Utenzi wa Mwana Kupona".

**Msimbo Uliotumika katika Kazi hii**

Katika mchakato wa uchambuzi wa takriri, mchambuzi hana budi kutumia msimbo ambao utamrahisishia katika uwasilishaji wa data zake. Katika kazi hii msimbo ufuatao umetumika:

NL=Neno lile lile
NS=Neno kisawe
NJI=Neno Jumuishi
NJW=Neno Jumuishwa
NJ=Neno Jumla

**Muhtasari wa Matini Teule**

Ili kuweza kuchambua takriri katika matini zilizoteuliwa mchambuzi hana budi kujua maana za hizo matini anazozichambua. Sehemu inayofuata itaeleza kwa ufupi maana zilizopo katika matini zilizoteuliwa.

***Matini I* -"Hadithi ya Mzee"**

"Hadithi ya Mzee" ni shairi la kisasa ambalo limetungwa na E. Kezilahabi katika Kichomi (1974).
Kama kichwa cha habari kinavyodokeza shairi hili ni hadithi ambayo mzee/ babu anaisimulia kwa watoto. Hadithi hii inahusu wavamizi waliokuja Afrika, na nzige wametumika kisitiari kama wavamizi. Walikula kila kitu ikiwa ni pamoja na utajiri wa watu. Watu hawakuwapenda hivyo waliwafukuza. Ingawa walikimbia lakini vilibaki vizalia vyao huku Afrika.

***Matini II* -"Nimekaribishwa Pombe"**

Hili ni shairi la kimapokeo ambalo limetungwa na R.H. Mlanzi. Shairi hili linazungumzia mtu ambaye amekaribishwa pombe na mpendwa wake na kujikuta kwenye mazingira tata. Kwa mfano, mtu huyu anakaribishwa

pombe lakini hajawahi kutumia pombe, na wakati huo huo chumbani alimokaribishwa anamkuta mwanamke; mazingira haya yanamfanya awe kwenye mgongano wa mawazo na anaomba ushauri afanye nini?

***Matini III* - "Utenzi wa Mwana Kupona"**
Utenzi wa Mwana Kupona ni wosia kutoka kwa Mwana Kupona Binti Mshamu ambaye ni mgonjwa kwa wakati huu na anautoa kwa bintiye Hashima Binti Mataka. Mama anamuusia kuhusu mambo mbalimbali ambayo aliona kuwa yangemsaidia hapa duniani hata kufika kifo chake.

**Data ya Uchambuzi**
Uchambuzi wa takriri unaanza na uchanganuzi ambao unabainisha aina mbalimbali za takriri na kiwango cha ujitokezaji cha kila aina. Aina ambazo zitazingatiwa ni zile zilizotajwa hapo juu, yaani: neno lile lile (NL), neno kisawe (NS), neno jumuishi (NJI), neno jumuishwa (NJW), neno jumla (NJ). Hatua hizi za uchambuzi hazikuonyeshwa hapa, kwa ajili ya kuokoa nafasi. Kilichoonyeshwa ni matokeo tu, ambayo yameonyeshwa katika majedwali 1 hadi 4.

Jedwali 1 linaonyesha "Msambao wa aina ya takriri katika Makala teule za Ushairi wa Kiswahili na kiasi cha asilimia".
Jedwali 2 linaonyesha Umbali wa takriri katika "Hadithi ya Mzee".
Jedwali 3 linaonyesha Umbali wa takriri katika "Nimekaribishwa Pombe".
Jedwali 4 linaonyesha Umbali wa takriri katika "Utenzi wa Mwana Kupona"

Maana ya matokeo hayo inajadiliwa hapa chini.

**Jedwali 1: Mtawanyo wa aina ya takriri katika Makala teule za Ushairi wa Kiswahili na kiasi cha asilimia**

| Aina ya takriri ya kimsamiati | Matini I | Matini II | Matini III | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Nl | 116<br>31.436% | 103<br>27.913% | 150<br>40.650% | 369<br>100% |
| Ns | 13<br>27.659% | 4<br>8.510% | 30<br>63.829% | 47<br>100% |
| Njw | 3<br>37.5% | 2<br>25% | 3<br>37.5% | 8<br>100% |
| Nji | 2<br>66.666% | 0<br>0% | 1<br>33.333% | 3<br>100% |
| Nj | 3<br>33.333% | 1<br>11.111% | 5<br>55.555% | 9<br>100% |
| Jumla | 137 | 110 | 189 | 436 |
| Asilimia | 31.422% | 25.229% | 43.348% | 100% |

**Yatokanayo na Data**

Data iliyowasilishwa hapo juu inaonesha kuwa utenzi una idadi kubwa ya takriri ya kimsamiati, ukifuatiwa na matini ya kwanza, na mwisho matini ya pili. Tukichunguza matini hizi na uwiano wa utokeaji wa aina mbalimbali za takriri ya kimsamiati tunaweza kusema kuwa urefu wa matini au wingi wa mishororo huashiria pia idadi kubwa ya aina za takriri ya kimsamiati. Hali hii inatupa picha kuwa takriri ni kipengele muhimu katika ushairi wa Kiswahili ambacho kinatumiwa na wasanii katika kazi zao. Aidha katika kuangalia aina ya takriri ya kimsamiati ambayo imejitokeza zaidi tunagundua kuwa takriri ya neno lile lile ndiyo imetumika zaidi ikifuatiwa na neno kisawe, neno jumuishwa, neno jumla na mwisho neno jumuishi. Sababu za matumizi haya tunaweza kuzipata kwa kuzingatia mada na muktadha wa matini zenyewe. Hata hivyo, baada ya kuchunguza data ambayo imetokana na usomaji wa matini pamoja na kubainisha utokeaji wa takriri ya kimsamiati tumeona kuwa kuna ufanano na utofautiano wa utokeaji wa vipengele hivi.

**Ufanano katika Utumizi wa Ushikamani wa Kimsamiati katika Matini Teule**

Kwa mujibu wa matokeo ya uchanganuzi (taz.jedwali 1), imeonekana kuwa matini zote zinatumia zaidi ushikamani wa aina ya neno lilelile (NL) kwa kiasi kikubwa na kufuatiwa na neno kisawe (NS), neno jumla (NJ) na neno jumuishwa (NJW). Aidha kuna matumizi hafifu sana ya neno jumuishi (NJI)

**Utofauti katika Utumizi wa Ushikamani wa Kimsamiati katika Matini Teule**

Katika matini zilizochanganuliwa imeonekana kuwa marudio au takriri nyingi katika utenzi hutokea baada ya mishororo kumi na mmoja na kuendelea, tofauti na mashairi ambayo yanatumia takriri zaidi katika mishororo isiyozidi minne (taz. Jedwali 2 ). Hali hii inaweza kuelezeka kuwa kwa kawaida mishororo ya utenzi ni mifupi kuliko ya mashairi[4]. Aidha kwa upande wa mashairi kutumia zaidi takriri katika mishororo minne ni kuleta ushikamani wa wazo na pia kuleta msisitizo. Tofauti na sentensi za lugha ambazo hubeba wazo au taarifa, kwa upande wa ushairi kwa kawaida wazo hubebwa kwenye ubeti (angalia jedwali 2-4)[5].

*Jedwali 2: Umbali wa takriri*

*Matini I– "Hadithi ya Mzee"*

---

[2] Dai hili linatokana na data zilizotumika katika makala hii.

[3] Utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kutumia data kutoka katika nathari ili kuona kama matokeo yatukuwa sawa au tofauti.

| Nambari ya mshororo | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko karibukaribu | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko katika umbali wa kuanzia mishororo 0-4 | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko katika aumbali wa kuanzia mishororo 5-10 | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko katika umbali wa mishororo 11 na zaidi |
|---|---|---|---|---|
| Jumla | 32 | 58 | 35 | 42 |
| Asilimia | 19.161% | 34.730% | 20.958% | 25.149% |

*Jedwali 3: Umbali wa takriri*

**Matini II - "Nimekaribishwa Pombe"**

| Nambari ya mshororo | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko karibukaribu | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko katika umbali wa kuanzia mishororo 0-4 | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko katika aumbali wa kuanzia mishororo 5-10 | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko katika umbali wa mishororo 11 na zaidi |
|---|---|---|---|---|
| Jumla | 21 | 81 | 14 | 11 |
| Asilimia | 16.535% | 63.779% | 11.023% | 8.661% |

*Jedwali 4: Umbali wa takriri*

**Matini III - Utenzi wa Mwana Kupona**

| Nambari ya mshororo | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko karibukaribu | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko katika umbali wa kuanzia mishororo 0-4 | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko katika aumbali wa kuanzia mishororo 5-10 | Ushikamani miongoni mwa mishororo iliyoko katika umbali wa mishororo 11 na zaidi |
|---|---|---|---|---|
| Jumla | 21 | 68 | 23 | 98 |
| Asilimia | 10% | 32.380% | 10.952% | 46.666% |

***Matini I*** -Hadithi ya Mzee

Katika shairi hili watoto wanamwomba babu awasimulie hadithi ya nzige. Kabla ya kuwasimulia hadithi yenyewe, babu anawaeleza kwanza kile alichokijua kuhusu wadudu hao. Anawaambia jinsi alivyopata habari za wadudu hawa kabla hajawaona kwa macho yake, sehemu waliyokuwapo kabla ya kuja Tanzania bara na tabia za wadudu hao. Baadaye anawaeleza hadithi yenyewe ya nzige.

Katika shairi hili maneno **hadithi, tusimulie, wadudu, nzige**, **walisema, watoto walafi, wamekuja, mzee** n.k. yamerudiwa sana. Maneno hayo ndiyo yanayotupa picha ya shairi. Mshairi anaanza kurudia neno **tusimulie** na **hadithi** yakifuatiwa na alama ya mshangao kuonesha/kusisitiza lengo la watoto. Neno **tusimulie** limerudiwa katika mistari ifuatayo: 7 na 8 Neno

**hadithi** limerudiwa katika mstari wa 7, 14, 15, 24 na 185. Watoto wana shauku ya kujua kile kilichotokea hivyo marudio haya yanaonesha shauku ya watoto. Si hivyo tu, wanataka pia kuhakikisha kama kweli kile wanachokifahamu ni cha kweli. Wana uhakika kuwa babu ndiye mwenye kujua. Neno **mzee** linarudiwa kuonesha msimulizi wa hadithi ni mtu wa aina gani (angalia mstari wa 9 na 179). Kama tunavyofahamu watu wengi wanaamini kuwa wazee ndio watu wenye busara na wanafahamu mambo yaliyotokea zamani. Aidha wazee husimama kama kiwakilishi cha maandishi hasa kwa wakati ambao hakuna kumbukumbu ya mambo yaliyotokea zamani.

Kiini cha hadithi hii ni jinsi nzige (wakoloni) walivyoingia Tanzania Visiwani na Tanzania Bara na kuvamia maeneo hayo pamoja na athari zao. Mshairi anarudia neno **nzige** mara nyingi ili kuonesha kiini cha hadithi au wazo kuu la hadithi.

Kabla ya hadithi yenyewe kuna usimulizi usio wa ushuhuda anaoutoa babu kuhusu wadudu ambao walivamia eneo la jirani kabla ya kufika katika eneo lao. Maneno **kwamba, habari, wengine** yamerudiwa ili kuonesha/kudokeza usimulizi huu.. Babu alikuwa anaeleza kile ambacho alikisikia kwanza kuhusu wadudu nzige. Maneno **walisema** na **kwamba** yanaonesha dhamira hii. Jambo hili pia linaweza kuthibitishwa kwa kuangalia njeo zilizotumika katika vitenzi hivyo. Tunaona kuna njeo ya wakati uliopita-**li**-, pamoja na –**ka**- inayoonesha usimulizi wa kimfuatano wa matukio –yaliyopita mfano. Wa**li**sema, tu**ka**ambiwa na wakatueleza. Maneno **wengine** na **walisema** yanaonesha kuwa babu hakuyashuhudia matukio hayo ndiyo maana anaiondoa nafsi yake katika usimulizi na kutumia nafsi ya tatu wingi.

Nzige walikaa kwa mara ya kwanza Pwani hivyo neno **Pwani** linarudiwa kuonesha wazo hili. Aidha mwanzoni watu hawakujua kama wadudu waliovamia eneo la Pwani walikuwa ni nzige. Habari zilizovuma zilikuwa zinahusu tu wadudu bila kujua aina ya wadudu hao. Neno **wadudu** linarudiwa kuonesha wazo hili. Neno **wadudu** limerudiwa katika mistari ifuatayo: 29,48, 65 na 111. Wadudu ni neno jumuishi ambalo linajumuisha aina mbalimbali za viumbe hao ambamo tunakuta nzige kama hiponimia. Kwa kutumia uhusiano huu wa neno jumuishi na neno jumuishwa kunafanya hadithi hii iwe na mtiririko mzuri na kuifanya hadhira ipate picha ya jumla kabla ya kupata picha halisi ya wadudu ambao wamelengwa katika hadithi wanayoitaka watoto. Vile vile kwa kutumia ushikamani wa neno jumuishi na jumuishwa kunaendana sambamba na maoni mbalimbali yaliyotolewa na wakazi wa eneo la babu; kwani waliweza kutoa tabia tofauti za wadudu pamoja na rangi zao bila kuwa na uhakika. Neno **wengine** limerudiwa ili kuonesha makundi tofauti ya watu na mawazo yao tofauti. Ubeti ufuataо unatupa picha halisi.

> Wengine walisema ni wekundu
> Wengine walisema ni weupe
> Wengine walisema ni walafi

Katika mstari 111 mshairi anarudia neno **wadudu** na anatupa wazo jipya

kuhusu wadudu hao. Usiku wakati watu walipokuwa wamelala wadudu hao walisikika wakila kama mchwa na walikuwa na pua ndefu. Huenda kwa wale watoto bado watakuwa na wazo lile lile la wadudu lakini kwetu sisi wasomaji hawa wadudu ni viumbe wenye maumbile ya binadamu.

Jambo hili linakuja kujidhihirisha kuwa **wadudu** wametumiwa kisitiari na kuwa ni binadamu pale babu anaposimulia hadithi ya nzige ambayo ni hadithi ya wavamizi walioivamwa nchi yetu na jinsi watu walivyopigana nao. Marudio rudio ya maneno na vifaa vilivyotumika kuwapiga hawa wadudu vinaonesha kuwa wadudu ni binadamu. Katika hali halisi mtu hawezi kutumia vifaa hivi kumwangamiza mdudu bali atatumia sumu n.k. Pia wadudu hawatumii lugha katika kuwasiliana ili wanatumia ishara na hisia.

Sinonomia zilizotumika ni pamoja na **walafi** kwa maana ya **walao kila kitu** na **kila wakati**, wamekuja kwa **kumefika**, **wanadamu kwa watu**, **mishale** kwa **mikuki**, na **vimatu** kwa **watoto wa nzige**. Maneno haya yametumika kama msisitizo ili kuleta uwiano wa wazo linalozungumziwa kutokana na ukweli kuwa jamii fulani za lugha zinapishana katika matumizi ya maneno.

Maneno jumuishwa (hiponimia) ambayo yametumika ni pamoja na **babu** ambalo linajumuishwa kwenye neno **mzee**. Neno hili limetumika ili kuonesha kuwa msimulizi ni mzee wa kiume na si mzee wa kike. Maneno mengine ni **ngao** ambalo linajumuishwa katika **zana**, **nzige** na **mchwa** yanayojumuishwa katika **wadudu** n.k. Kwa kutumia maneno jumuishwa mshairi anataka hadhira ipate ile dhana mahsusi ya kinachozungumziwa.

Maneno jumuishi yaliyotumika ni pamoja na **silaha** ambalo linajumuisha **ngao,** mishale, mikuki. Matumizi ya maneno jumuishi yanamfanya mtu apate picha ya jumla na awe na uhuru wa kufikiri na kuoanisha vitu vingi zaidi.

Maneno jumla yaliyotumika ni **mazao** kwa **majani** mst.154 na 152, **wanyonyaji** mstari 106 kwa **nzige** mstari 90 na **wana** mstari 139 kwa **watoto** mstari 21. Kwa kutumia maneno jumla hadhira inapata picha halisi ya kitu pamoja na utambulisho tofauti wa kitu hicho mfano **wanangu** kwa maana ya watoto katika jamii za Kiafrika ni mali ya jamii. Vile vile **wanyonyaji** lina maana ya viumbe ambao wanaishi kwa kutegemea jasho la kiumbe mwingine.

***Matini II*** **- Nimekaribishwa Pombe**

Mshairi anaeleza jinsi ilivyokuwa. Yeye alikuwa safarini kwenda kwa rafiki yake, kabla ya kufika nyumbani kwa huyo rafiki anakutana na huyo rafiki mkuu (shoga) na anamkaribisha kilabuni. Si hivyo tu, mle kilabuni anamwingiza chumbani na anamkuta mwanamke hivyo wote wawili wanahudumiwa bia. Yule mwanamke anakunywa bia yake ila huyu mgeni anashindwa. Isitoshe shoga yake anamtoroka na anawaacha wawili tu

chumbani, yeye na yule mwanamke. Mwanzoni huyu mwanamke alikuwa amevaa ushungi lakini baadaye anauvua Hivyo huyu kijana hajui afanye nini. Hawezi kunywa pombe kwani hajawahi kunywa pombe na anaogopa wenzake watasemaje endapo atainywa ile pombe. Pia anaogopa kuwa endapo ataondoka na kumwacha huyu mwanamke atamuudhi shoga yake, hivyo anabaki analia.

Shairi hili limetumia takriri ya maneno yale yale kwa kiasi kikubwa, sinonimu, hiponimia na maneno jumla katika kufikisha ujumbe wake. Marudiorudio ya maneno yale yale yametumika ili kuonesha wazo kuu la shairi. Maneno **nimekaribishwa, pombe, nifanyeje** yamerudiwa sana na ndiyo yanayobeba wazo kuu la shairi. Kwa mfano marudio ya neno **nimekaribishwa** tunayapata katika mistari ifuatayo: 7, 8, 12, 16, 20, 28, 32, 36na 44. Neno pombe limerudiwa katika mistari ifuatayo: 8, 12, 16, 20, 24, 26, 28, 32, 35, 36, 40 na 44. neno nifanyeje ambalo linaonesha hali ya kutokuwa na uamuzi binafsi limerudiwa katika mstari wa 4, 8, 12, 16, 20, 24, 28, 32, 36, 40 na 44

Rafiki amekuwa ni chanzo cha matatizo yaliyompata mshairi. Neno **rafiki** limerudiwa mara mbili tu kama mchomozo. Katika hali halisi tulitarajia neno hili litokee mara nyingi lakini sivyo. Mshairi amerudia neno rafiki kuonesha dhamira hii. Kwa kawaida tunamchukulia rafiki kama msaada wetu mkubwa. Hata hivyo mshairi kupitia shairi hili anaonesha kuwa rafiki zetu wanaweza kutusababishia matatizo kama yaliyompata huyu mgeni na kufikia hatua ya kutowaamini tena marafiki. Hivyo kupitia takriri hii tunaambiwa kuwa tusimwamini kila rafiki. Hii inajidhihirisha wazi tunapomwona mgeni akiomba ushauri kwa ndugu zake na si kwa rafiki zake. Hivyo mgeni huyu anatafuta suluhisho kwa watu wengine. Baada ya kusongwa na mawazo mshairi anawauliza watu mbalimbali mmojammoja au kama kundi. Maneno **ndugu yangu/zangu, mwenzangu/wenzengu** yamerudiwa ili kuonesha makundi ambayo mshairi anayaomba msaada. Mfano maneno **ndugu yangu/zangu** yamerudiwa katika mistari ifuatayo:5, 8, 12, 16, 20, 24, 28, 32, 36, 40, 41 na 44. Aidha neno **mwenzangu/wenzangu** limerudiwa katika mstari wa 6, 11,15,17,18,26,27,30 na 39.

Mwaliko wa kilabuni ulifuatwa na matukio mengi ya mfululizo. Mshairi amerudia neno **na** kuonesha mfuatano huu wa matukio. **Na** ni kiunganishi (neno linalotumika katika kuonesha nyongeza).
Mfano:

> Kanikaribisha chini, kiti cha chake *na* changu
> Kisha akaoda bia, chupa ya kwake *na* yangu
> Mezani kaniwekea chupa ya kwake *na* yangu
> *Na* mara akafungwa, chupa ya kwake *na* yangu.

Tunaona kuwa **na** limetumika kwa hali ya uchomozo hasa tunapochunguza mazingira ya kawaida ya kutumia neno hili. Kwa kawaida sentensi za Kiswahili hazianzi kwa kutumia neno **na**, lakini katika mfano wa hapo juu, tunaona kuna ukiukwaji wa mfuatano wa maneno katika sentensi na neno

**na** limetumika mwanzoni mwa sentensi. Neno **na** limerudiwa pia katika mistari ifuatayo: 7, 9, 10, 13, 15, 19, 25, 35, 37, 38, 39 na 41.

Mshairi pia ametumia sinonimu katika kusisitiza mawazo yake. Mfano **shoga** kumaanisha **rafiki** mstari wa 2 na 43, **nimekirimiwa** badala ya **nimekaribishwa**, **kuonja** bia badala ya **kunywa** bia. Dhima ya matumizi haya ya sinonimu ni kuleta uwiano wa maana.

Katika shairi hili pia kuna matumizi ya hiponimia. Kwa mfano matumizi ya neno **bia** mstari 9. Kwa kutaja neno **bia** ambalo ni neno jumuishwa katika pombe mshairi anataka kuonesha aina maalum ya pombe ambayo mgeni huyu amekaribishwa. Ni kwamba anaondoa aina nyingine za pombe ambazo hadhira wanazifahamu.

Maneno jumla kama vile mama yametumika. Neno **mama** limetumika ili kumrejelea Seketa ambaye ni mwanamke aliyeachwa chumbani pamoja na mgeni. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004:219) inafafanua neno **mama** kama mzazi wa kike. Maana nyingine za ziada za neno mama ni mtu mke ambaye si msichana, yaani mwenye umri mkubwa. Kwa mshairi kumwita Seketa mama kunamaanisha kuwa Seketa ni sawa au ana umri pengine sawa na wa mamake mzazi. Hivyo mgeni na Seketa wanapishana sana kiumri.

***Matini III* – Utenzi wa Mwanakupona**

Mambo muhimu ambayo mama anamweleza binti yake ni pamoja na kufungamana na sheria na taratibu za dini yake, kuwa na heshima po pote pale atakapokwenda, kuwa mwaminifu na mnyenyekevu, kuheshimu watu wote hasa wakubwa, awe mtu wa furaha lakini asiwe mhojaji sana, asishirikiane na wajinga (ambao hawamwamini Mungu) kwani watamharibia maisha yake. Vilevile anamwambia kuwa mtu muhimu kuliko wote katika maisha yake ni mume wake kwa maisha ya hapa duniani na ahera hivyo anapaswa amheshimu sana, asijibizane naye, anachotaka mumewe ampatie, amfurahishe, alalapo asimwamshe ila awe pembeni mwake hadi atakapoamka mwenyewe, ahakikishe anamfanyia usafi ikiwa ni pamoja na kumnyoa ndevu na kumkanda. Pia anaambiwa kuwa ni lazima awe msafi na ajirembe. Mwisho anaambiwa awaheshimu watu wake na wageni watakaokwenda kumtembelea.

Utenzi huu umetumia aina zote za takriri ya kimsamiati katika kuwasilisha dhamira mbalimbli kwa hadhira. Kuna marudio ya maneno yale yale kama vile **mwanangu, mola**:, **mumeo, ahera, akinena** na hali tofauti tofauti za neno **ambia** kama vile **kukwambia**, **nimekwambia**, **nakwambia** kwa madhumuni ya kusisitiza ujumbe wake kwa hadhira. Binti kazi yake kubwa ni kupokea kile anachoambiwa ndiyo maana tunaona msisitizo huu kwa kurudia neno **ambia**. Hatakiwi kufanya majadiliano yo yote ama na mama yake au na mumewe ndiyo maana hakuna hali ya kutendana isipokuwa hali ya kutendewa tu.

Neno **mwanangu** limerudiwa lakini mara mbili tu mstari wa 42 na 57. Huu

ni mchomozo. Katika hali ya kawaida tulitarajia neno hili lirudiwe mara nyingi hata kuliko maneno yote ili kuonesha upendo wa mama kwa mtoto hasa kutokana na hali ya ugonjwa aliokuwa nao mama.

Hapa msanii anawafanya wasomaji wajiulize maswali ya "kwa nini?" Msanii anataka kuwasilisha kwa hadhira majukumu ya binti huyu. Binti sasa ni mkubwa na watu wengine kama vile mumewe watamtegemea. Sasa atakuwa ni mali ya mumewe na ya jamii nzima. Pia anataka kuonesha kuwa ingawa Hashima ni mtoto wa Mwana Kupona majukumu ya mama kwa mtoto sasa yamefikia mwisho na huu wosia huenda ni wajibu wa mwisho wa mama kwa mtoto wake. Mama anataka kuweka umbali fulani wa mahusiano baina yake na bintiye.

Sinonimu pia zimetumika ili kusisitiza kile ambacho msanii amekieleza. Aidha, sinonimu zimetumika ili kuleta uwiano wa maana. Baadhi ya maneno haya ni kama vile **simjibu** mstari 111 badala ya **kuinyamalia** mstari 72 na **kunyamaa** mstari 112, **daima** mstari 224 badala ya **milele** mstari 222, **mvuli** mstari 225 badala ya **mume** 102, **binadamu** badala ya **mtu**. Pia neno binadamu limetumika katika kuonesha maana ya ziada kwamba si watu wote ambao wana ubinadamu.

**Hitimisho**

Makala hii imetoa picha halisi ya uchambuzi wa takriri hasa katika kazi za fasihi. Aidha imetoa ufafanuzi kuhusu dhana nzima ya takriri na hatimaye kuonesha jinsi ya kuchambua takriri ya kimsamiati katika Ushairi wa Kiswahili.

Katika uchambuzi wa takriri ya kimsamiati tumeona kuwa matumizi ya marudiorudio ya maneno yale yale ni kwa ajili ya kuonesha wazo kuu au dhamira kuu iliyoko katika matini. Aidha sinonimua hutumika katika kusisitiza dhamira kuu pamoja na kuleta uwiano wa maana. Kwa upande wa hiponimia hutumika katika kuonesha jambo mahsusi wakati neno jumuishi na neno jumla huonesha jambo la jumla na upana wa jambo linalojadiliwa. Kwa ujumla takriri inaweza kutusaidia katika kupata maana au kushadidia maana katika matini. Hii ina maana kwamba tunaweza kupata maana inayowasilishwa na matini na kuchunguza jinsi takriri inavyoshadidia maana hiyo, au tukachunguza jinsi takriri inavyohusika katika kuibua maana katika matini. Kutokana na data zetu tunaona kuwa takriri ni kipengele kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao. Tunaweza kutoa tamko kuwa ukubwa wa kazi au wingi wa mishororo au mistari iliyoko katika matini huashiria pia matumizi makubwa ya takriri.

Kwa kumalizia, tutataja mipaka ya makala na kueleza jinsi utafiti huu unavyoweza kupanuliwa. Makala hii imeweza tu kuchambua takriri katika ushairi wa Kiswahili kwa kutumia mashairi mawili tu na utenzi mmoja. Ushairi wa Kiswahili ni zaidi ya tungo hizi.Hivyo uchambuzi wa takriri ungeweza kupanuliwa ukazingatia kumbo zote za ushairi. Aidha, takriri

ni mchomozo. Katika hali ya kawaida tulitarajia neno hili lirudiwe mara nyingi hata kuliko maneno yote ili kuonesha upendo wa mama kwa mtoto hasa kutokana na hali ya ugonjwa aliokuwa nao mama.

Hapa msanii anawafanya wasomaji wajiulize maswali ya "kwa nini?" Msanii anataka kuwasilisha kwa hadhira majukumu ya binti huyu. Binti sasa ni mkubwa na watu wengine kama vile mumewe watamtegemea. Sasa atakuwa ni mali ya mumewe na ya jamii nzima. Pia anataka kuonesha kuwa ingawa Hashima ni mtoto wa Mwana Kupona majukumu ya mama kwa mtoto sasa yamefikia mwisho na huu wosia huenda ni wajibu wa mwisho wa mama kwa mtoto wake. Mama anataka kuweka umbali fulani wa mahusiano baina yake na bintiye.

Sinonimu pia zimetumika ili kusisitiza kile ambacho msanii amekieleza. Aidha, sinonimu zimetumika ili kuleta uwiano wa maana. Baadhi ya maneno haya ni kama vile **simjibu** mstari 111 badala ya **kuinyamalia** mstari 72 na **kunyamaa** mstari 112, **daima** mstari 224 badala ya **milele** mstari 222, **mvuli** mstari 225 badala ya **mume** 102, **binadamu** badala ya **mtu**. Pia neno binadamu limetumika katika kuonesha maana ya ziada kwamba si watu wote ambao wana ubinadamu.

**Hitimisho**

Makala hii imetoa picha halisi ya uchambuzi wa takriri hasa katika kazi za fasihi. Aidha imetoa ufafanuzi kuhusu dhana nzima ya takriri na hatimaye kuonesha jinsi ya kuchambua takriri ya kimsamiati katika Ushairi wa Kiswahili.

Katika uchambuzi wa takriri ya kimsamiati tumeona kuwa matumizi ya marudiorudio ya maneno yale yale ni kwa ajili ya kuonesha wazo kuu au dhamira kuu iliyoko katika matini. Aidha sinonimua hutumika katika kusisitiza dhamira kuu pamoja na kuleta uwiano wa maana. Kwa upande wa hiponimia hutumika katika kuonesha jambo mahsusi wakati neno jumuishi na neno jumla huonesha jambo la jumla na upana wa jambo linalojadiliwa. Kwa ujumla takriri inaweza kutusaidia katika kupata maana au kushadidia maana katika matini. Hii ina maana kwamba tunaweza kupata maana inayowasilishwa na matini na kuchunguza jinsi takriri inavyoshadidia maana hiyo, au tukachunguza jinsi takriri inavyohusika katika kuibua maana katika matini. Kutokana na data zetu tunaona kuwa takriri ni kipengele kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao. Tunaweza kutoa tamko kuwa ukubwa wa kazi au wingi wa mishororo au mistari iliyoko katika matini huashiria pia matumizi makubwa ya takriri.

Kwa kumalizia, tutataja mipaka ya makala na kueleza jinsi utafiti huu unavyoweza kupanuliwa. Makala hii imeweza tu kuchambua takriri katika ushairi wa Kiswahili kwa kutumia mashairi mawili tu na utenzi mmoja. Ushairi wa Kiswahili ni zaidi ya tungo hizi.Hivyo uchambuzi wa takriri ungeweza kupanuliwa ukazingatia kumbo zote za ushairi. Aidha, takriri

inaweza pia kuchambuliwa pia katika nyanja nyinginezo za kama vile katika riwaya, semi na fani nyinginezo za maandiko. Bila shaka matokeo ya uchambuzi huu, hasa ukiwa wa kiulinganishi, yatazidi kutoa mwanga kuhusu dhana hii ya takriri.

### Marejeleo


Chacha, C.N. 1992. *Ushairi wa Abdilatif Abdallah: Sauti ya Utetezi.* Dar es Salaam: Dar Salaam University Press.

Crowll, M.W. 1966. *Style, Rhetoric and Rhythm.* Princeton: Princeton University Press.

Enkvist N.E., S.John and G. Michael. 1964. *Linguistics and Style.* Oxford: Oxford University Press.

Enkvist, N.E., 1973. *Linguistic Stylistics.* The Hague & Paris: Mouton.

Finnegan, R. 1977. *Oral Poetry: Its Nature, Significance, and Oral Context.* Cambridge: Cambridge University Press.

Gutwinski, W. 1976. *Cohesion in Literary Texts: A Study of Some Grammatical and Lexical Features of English Discourse.* The Hague: Mouton.

Halliday, M.A.K. and Hasan, R. 1976. *Cohesion in English.* London: Longman.

Kahigi, K.K. 1997. 'Structural and Cohesion Dimension of Style: A Consideration of Some Swahili Texts in Maw 1974' *Journal of Linguistics and Language in Education.* (New series) Vol.3: 1–79, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu.

Kahigi, K.K. and Mulokozi, M.M. 1976. *Malenga wa Bara.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Mulokozi, M.M. and Kahigi, K.K. 1979. *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Kandoro, S.A. 1972. *Mashairi ya Saadani.* Dar es Salaam: Mwananchi Publishing (1966) Ltd.

Kezilahabi, E. 1974. *Kichomi.* Nairobi: Heinemann Educational Books (E.A) Ltd.

__________ 1976. *Ushairi wa Shaaban Robert.* Nairobi: Longman.

Khatibu, M. S. 1986. 'Tamathali za Semi za Kiswahili'. *Mulika* Na.18 Pp 16-28.Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

King'ei, G.K., 1987. 'Usanifu wa lugha katika uandishi wa Ebrahim Hussein' *Mulika.* Na.19: 19 -35, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Leech, G.N. 1969. *A Linguistic Guide to English Poetry.* London: Longman.

Lyimo, E.B. (2004). Reiteration in Kiswahili Poetry .Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Materu, F. Mushi, C.B. and Njau, I.1986. 'Tendehogo'. *Mulika* Na.18:41-45. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Materu, F. Mushi, C.B. and Njau, I. 1986. 'Hawala ya Fedha'. *Mulika* Na.18:46-51. Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mlacha, S.A.K. 1984. 'Riwaya za Visiwani (1970-1980) na Ujenzi wa Jamii Mpya'.

*Mulika* Na.16:4-31. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mponda, M S. 1988. 'Nyota ya Huzuni'. *Mulika* Na. 20:49-65. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Msokile, M. 1986 'Teuzi za Nafsi'. *Mulika*: Na.18:16-28. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, A.M.K., 1996 A Stylistic Comparison of Swahili Prose and Poetry: The Case of Lexical Cohesion. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (ed.) 1999. Tenzi Tatu za Kale. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mutembei, A.K. 1994. Phonological Aspects of Foregrounding in Kiswahili. (M.A. Dissertation). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mvungi, T.A. 1988. "Fungate ya Uhuru" *Mulika* Na.20:82-89. Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mwansoko H.J.M. 1991. *Mitindo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Nosek, J. 1969. "Pause and Repetition in Modern Colloquial English". *Acta Universitatis Carolinae – Philologica 3: Prague Studies in English* Vol. 13:35 –58.

Parker, A.C.1981. "Figures of speech in Swahili Proverbs: Repetition" *Makala za Semina za TUKI na Makala Mbalimbali za Wachunguzi.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Peer, W.V. 1986. *Stylistics and Psychology: Investigation of Foregrounding.* London: Crom Helm.

Persson, G. 1974. *Repetition in English: Part 1 Sequential Repetition.* Uppsala..

Robert, S.1991. *Kielelezo cha Fasihi.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Sanka, S.M. 1988. 'Tahakiki: Fungate ya Uhuru'. *Mulika* Na. 24:85-89. Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

__________1994. Semantic Deviation in Iraqw Oral Poetry (MA Dissertation).Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sebeok, T. (ed.) 1960. *Style in Language.* Cambridge, Mass: MIT Press.

Senkoro, F.E.M.K. 1982. *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

__________1984. 'Kasri ya Mwinyi Fuad'. Mulika Na. 16:32-35.Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

__________ 1988. *Ushairi, Nadharia na Tahakiki.* Dar es Salaam:Dar es Salaam University Press.

__________ 1988 'Shida'. *Mulika* Na.20:30-41. Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

__________ 1988. "Damu imemwagika". *Mulika* Na.20:42-48. Dar es salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Tandika, S.A. 1986. 'Kuli, Fimbo ya Mnyonge na Shida'. *Mulika* Na.18:18-30. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Ullmann, S. 1964. *Language and Style.* Oxford: Blackwell.